

MKATABA WA KUPANGISHA GODOWN CHUMBA NAMBA 3, BLOCK 'O', PLOT
NAMBA.51 OLD AIRPORT STREET, JININI MBEYA

Mkataba huu umetengenezwa na kuingiwa leo Tarehe 8 Mwezi Februari 2022

BAINA YA

MOVIN JOSEPH MWAHOLI wa S.L.P 1433 Mbeya, Simu namba 0754 376 452 (Ambaye katika Mkataba huu ataitwa “**MPANGISHAJII**”, jina ambalo litamaanisha kila mahali ambapo maudhui yake yataruhusu watendaji, wawakilishi na warithi wake) **KWA UPANDE MMOJA**

NA

KINGLION INVESTMENT COMPANY LIMITED kampuni binafsi ya S.L.P 15245 Dar es Salaam, Mwenye namba ya Mlipa Kodi 130-201-121 (Atakayefahamika kama “**MPANGAJI**” katika mkataba huu) **KWA UPANDE**

MWINGINE

KWAMBA Mpangishaji ni mmiliki halali wa Godown lililopo eneo la Old Airport, Block “O”, Plot No.51 Godown No.3 Halmashauri ya jiji la Mbeya (Ambapo kwenye mkataba huu litafahamika kama “Godown”).

KWAMBA Mpangaji ameonisha nia na kuridhia kutaka kupangishwa eneo hilo kama itakavyokuliwa katika mkataba huu.

NA KWAMBA Mpangishaji na Mpangaji kwa pamoja wamekubaliana kufanya makubaliano haya kama itakavyoandikwa hapa chini.

Hivyo, pande zote mbili zinashuhudia kwamba:

1. **Mpangishaji** anamkodisha Mpangaji Godown kwaajili ya biashara zake halali kwa kipindi cha miezi (36) toka siku ya kutia saina na kuingia kwenye Godown.
2. Mkataba huu utakuwa wa pango lenye thamani za Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi na Tano (TZS.15,000,000/=) tu kwa kipindi chote tajwa hapo juu. Kiasi hiki ni sawa na kodi ya TZS 1,250,000/= kwa mwezi.
3. Kwamba Mpangaji amekubali kulipa kiasi hicho chote kwa mkupuo mmoja kupitia benki akaunti ya Mpangishaji ambayo ni **CRDB BANK ACCOUNT NO: 0150362065700**
TAWI LA MBALIZI ROAD JINA: MOVIN JOSEPH MWAHOLI/FATUMA
M.MWAHOLI.
4. Kwamba malipo hayo ya pango hayatahusiana na ankara zote za maji, umeme, usafi, ulinzi na ukarabati wowote ambao Mpangaji ataufanya baada ya makubaliano haya. Mpangaji atalipa Ankara hizo na gharama nyingine kwa matumizi yake yeye mwenyewe.
5. Mpangishaji anampa mamlaka Mpangaji ya kuboresha na kurekebisha Godown kwa matumizi yake binafsi na kwa gharama zake.
6. Mkataba huu utafanyiwa marejeo baada ya muda wake kukamilika na Mpangishaji na Mpangaji kwa pamoja watakaa na kujadili maudhuo mapya ya kuendelea na mkataba huu.
7. Kwamba Mpangishaji anamuhakikishia Mpangaji kufurahia na kutumia Godown hilo bila

bugudha yoyote ile kutoka kwake au mamlak yoyote ile ya kiserikali na binafsi.

8. Kwamba Mpangaji atatumia Godown hilo kwa kusudi la kisheria na kufuata taratibu za mamlaka husika.
9. Endapo itatokea sintofahamu itayomfanya Mpangaji kutofanya shughuli zaake kama ilivyokubalika basi pande zote zitarudi kama zilivyokuwa awali kabla ya kutiliana saini mkataba huu.
10. Pande zote zimeafikiana endapo kutatokea kutoelewana basi wataketi na kujadiliana changamoto hizo.
11. Pande zote mbili zimekubaliana kukaa mara kwa mara kwa lengo la kujadiliana na kushauriana mambo yote yenye lengo la kukuza na kuboresha mkataba huu.
12. Pande yoyote itakayotaka kuvunja mkataba huu itatoa notisi ya siku thelathini (30) kabla yakufanya hivyo.
13. Mkataba huu unalindwa na kutafsiriwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama itatokea mgogoro basi pande zote zitaujadili.

HIVYO BASI, PANDE ZOTE ZINASHUHUDIA kwa kuweka saini zao katika tarehe na Mwaka kama inavyotokea hapa chini:

IMEWEKWA SAHIHI na KUWASILISHWA
hapa Mbeya na **MOVIN JOSEPH MWAHOLI**
ambaye ninamfahamu/ametambulishwa
kwangu na
.....ambaye ninamfahamu.
Leo Tarehe ... 8 ... Mwezi ... 2 ... 2022

Mbe

.....
MPANGISHAJI



Mbele yangu:

Jina: **ROBERT RENATUS RWEYEMAMU**
Saini:
Anwani: **P.O BOX 32196**
Wadhifa: **WAKILI**



IMEWASILISHWA NA KUPIGWA MUHURI
WA MOTO/STAMP ya KINGLION INVESTMENT
COMPANY LIMITED

Leo Tarehe ... 8 ... Mwezi ... 2 ... 2022
Jina: **JOHN MALALE EUAJ**
Saini:
Anwani: **P.O. BOX 15245 DJM**
Wadhifa: **SALES MANAGER**

John Malale Euj

.....
MPANGAJI

Mbele Yangu:

Jina: **ROBERT RENATUS RWEYEMAMU**
Saini:
Anwani: **P.O BOX 32196**
Wadhifa: **WAKILI**

